



Bi. Cheryl Watson-Harris, Msimamizi

Bi. Vickie B. Turner, Mwenyekiti wa Bodi
 Bw. Dijon DaCosta, Mwenyekiti Msaidizi
 Bi. Anna Hill
 Bw. Marshall D. Orson
 Bi. Deirdre Pierce
 Bi. Allyson Gevertz
 Dkt. Joyce Morley

MEDIA ADVISORY

Ijumaa, 5 Novemba 2021

Mawasiliano:

Portia Kirkland, 678-427-4898
 Carla Parker, 404-734-1717

WILAYA YA SHULE ZA KAUNTI YA DEKALB KUTANGAZA HATUA ZITAKAZOFUATA ZA MPANGO MKUU WA E-SPLOST, MIRADI NA MABORESHO YANAYOPENDEKEZWA YA SHULE

STONE MOUNTAIN, Ga. – Maafisa wa Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb watafanya mkutano Ijumaa, Nov. 8 ili kutangaza kuanzishwa kwa mpango mkuu unaoangazia maboresho ya miundomsingi na shule katika wilaya nzima utakaofadhiliwa na E-SPLOST mpya iliyoidhinishwa hivi karibuni (Education- Special Purpose Local Option Sales Tax).

LINI: Jumatatu, Nov. 8, 2:45PM

WAPI: DeKalb County School District, Administrative and Instructional Complex. 1701 Mountain Industrial Blvd, Stone Mountain, GA 30083

WANENAJI:

**Msimamizi wa DCSD Cheryl Watson-Harris Bodi ya Elimu ya DeKalb
 Mwenyekiti wa Bodi ya Elimu ya DeKalb Vickie Turner**

“Kama sehemu ya ahadi inayoendelea ya uwazi na kushirikisha, tunaendelea kualika jamii kusikia kuhusu miradi ya mabadiliko ambayo tumepanga kama sehemu ya kuendelea kwa ufadhili uliodhinishwa wa E-SPLOST,” alisema Msimamizi wa DeKalb Cheryl Watson-Harris.

Kuhusu E-SPLOST

Kura ya maoni ya E-SPLOST ilipitishwa tarehe 2 Novemba na wapiga kura wa Kaunti ya DeKalb na kupitishwa kwa asilimia 81 ya kura. E-SPLOST itatoza ushuru wa asilimia moja wa mauzo na matumizi kwa bidhaa na huduma zilizounuliwa katika Kaunti ya DeKalb kwa miaka mitano ijayo. E-SPLOST hii ni mwendelezo wa DCSD. Ukusanyaji wa fedha za E-SPLOST V utafanyika kuanzia Julai 2017 hadi Juni 2022. Ukusanyaji wa fedha za E-SPLOST VI umeratibiwa kutozwa kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2027. DCSD inakadiria ushuru utaleta dola milioni \$660 hadi dola milioni \$700 katika mapato na kufadhili miradi ya kuboresha shule na ya kuboresha mipango.

Miradi ya E-SPLOST inahusisha kujenga Shule mpya ya Upili ya Cross Keys; kuunda shule ya Sequoyah, ikiwemo shule mpya ya kati, shule ya upili, na shule ya msingi iliyo karibu ya Dresden; kubadilisha Shule ya Upili ya McNair kuwa Shule ya Kazi za Kiteknolojia (Career Tech Academy); kuchanganyisha shule za msingi za Dunair na Allgood kuwa shule mpya yenye kituo cha masomo ya watoto na kujenga upya Shule ya Msingi ya Hawthorne.

Miradi mingine inajumuisha kubadilisha Shule ya Upili ya Avondale na jengo na uwanja mpya ili iwe Shule ya Sanaa; kuanzisha Shule ya Teknolojia ya Mtandao na Uhandisi kwa kubadilisha Shule ya Upili ya Towers; kuunda upya Shule ya Msingi ya Dresden; kuunda upya Shule ya Msingi ya Stoneview; kuunda upya Shule ya Msingi ya Jolly, uundaji wa K-8 katika Shule ya Msingi ya Austin; vituo vya ziada vya elimu ya watoto; na maboresho ya ziada ya miundomsingi ya kiteknolojia.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea www.dekalbschoolsga.org/e-splost.

###